

**SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WAFANYAKAZI TANZANIA
(TUCTA)**

**SALAMU ZA NDUGU TUMAINI NYAMHOKYA, RAIS WA
SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WAFANYAKAZI TANZANIA
(TUCTA) KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA
USALAMA NA AFYA DUNIANI, 28 APRILI, 2019 MBEYA.**

**Mh. Jenista Mhagama, Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge,
Kazi, Ajira na Walemavu,**

Mh. Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya

**Ndugu Khadija Mwenda, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Afya
na Usalama Kazini, (OSHA).**

**Ndugu Jealous Chirove, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Shirika la Kazi
Duniani (ILO) Kanda ya Afrika Mashariki.**

**Ndugu Dan Sora Tandisi, Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa
Chama cha Waajiri Tanzania (ATE).**

Ndugu Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi,

Ndugu Wafanyakazi,

Mabibi na Mabwana.

Ndugu Mgeni Rasmi.

Kwanza kabisa napenda kukushukuru kwa dhati kwa kuhudhuria kilele cha MAADHIMISHO ya Siku ya Usalama na Afya Duniani.

Leo ni siku ya kuwakumbuka wafanyakazi wenzetu walioumia, kupata ulemavu na wengine kufariki kutokana na ajali au magonjwa wakati wakiwa kazini. Siku hii hutupa wasaa wa kutafakari madhara yanayotusibu sehemu zetu za kazi na namna ya kujikinga dhidi ya madhara hayo.

Kwa jumla sehemu za kazi zina vihatarish vingi na haziko salama kwa kiwango kinachotakiwa. Ukweli huu unadhihirishwa na takwimu mbali mbali pamoja na matukio ya ajali na maafa yanayotokea katika machimbo, viwandani na mashambani ambapo wafanyakazi wanapoteza maisha kwa sababu ya vihatarishi vinayotokana na kazi zisizo salama au mazingira yasiyo salama.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kwa kuzingatia Kauli mbiu ya maadhimisho ya Siku ya Usalama na Afya yam waka huu ammbayo inasisitiza umuhimu wa kuwa Usalama na Afya katika mustkabali wa Kazi kuelekea Uchumi wa Viwanda **ninapenda kutoa salamu za kutoa wito, kuwa wote tushirikiane kuhakikisha kuwa tunatimiza** wajibu wetu kwa kila mdau kuhakikisha kuwa mahali pa kazi pako salama.

Kwa upande wa Serikali ni wajibu wake na tunakumbusha kutekeleza mambo yafuatayo:

- i. Kuelekea uchumi wa Viwanda Serikali ihakikishe kwamba wawekezaji wote wanaokuja hapa nchini wanatimiza masharti ya Usalama na Afya kazini sambamba na shughuli wazifanyazo.

- ii. Serikali ipanue wigo wa elimu ya ufundi (Polytechnic Colleges) inayoshabihiana na uchumi wa Viwanda na kuweka Mitaala ya elimu ya Usalama na Afya katika mafunzo hayo pamoja na Shule za Sekondari.
- iii. Serikali iweke utaratibu ulio salama katika kuondoa (disposal) kemikali zenye sumu pamoja na kuhifadhi mazingira salama, ili kuzuia ongezeko la athari zitokanazo na uzalishaji Viwandani.

Kwa upande wa Waajiri, tunahimiza watekeleze yafuatayo:-

- i. Waanzishe na kuimarisha mipango ya mafunzo juu ya Afya na Usalama kwa wafanyakazi wao.
- ii. Waweke utaratibu wa ukaguzi wa afya wa mara kwa mara (periodic medical examination) kwa wafanyakazi wao.
- iii. Vilevile waunde Kamati za Afya na Usalama katika sehemu zote za kazi hapa nchini na kuhakikisha kwamba zinafanyakazi ya kuboresha Afya na Usalama wa Wafanyakazi.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) kwa kushirikiana na wafanyakazi wote nchini linaahidi kuwa litashirikiana kikamilifu wakati wote katika jitihada zote za kuhakikisha mahali pa kazi panakuwa salama ili kulinda nguvu kazi kwa maendeleo ya taifa letu.

Mwisho nitumie nafasi hii kupongeza viongozi na wafanyakazi wa Mamlaka ya Usalama na Afya (OSHA) kwa kazi nzuri wanayoendelea kuifanya kuchangia hali ya usalama mahali pa kazi.

NAWASHUKURU KWA KUNISIKILIZA.

RAIS WA TUCTA